

Kiongozi kwa Watumiaji wa Dodoso la Ufuatiliaji Utawala Bora katika Misitu

Imetayarishwa na
Elida Fundi Ishabakaki

Januari 2012



Washiriki katika zoezi la ufuatiliaji utawala bora katika sekta misitu- Kijiji cha Mayo,
wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga

Utangulizi

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya wanamtandao wa MJUMITA wanaoteuliwa kufanya zoezi la ufuatiliaji utawala bora kwa kutumia “dashboard” inayojumuisha maswali mbalimbali yanayohusu usimamizi wa misitu pamoja na nguzo za utawala bora katika sekta ya misitu kama vile utawala wa sheria zinazosimamia misitu, uwajibikaji, ushirikishwaji, utoaji maamuzi na uwazi. Kiongozi hiki cha mtumiaji kinatoa mwongozo ambao ni rahisi kutumiwa na wana MJUMITA watakaofanya zoezi la kukusanya taarifa kwa ajili ya kufuatilia utawala bora ngazi ya kijiji.

“Dashboard” ni mfumo unaotumika kufanya tathmini ya kiwango cha utawala bora katika mipango ya uhifadhi wa misitu kwenye jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu Tanzania. Mfumo huu utatumika kuchunguza yafuatayo;

- Kiwango cha uwazi katika shughuli za usimamizi wa misitu na matumizi ya fedha,
- Ushirikishwaji wa jamii katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na misitu wanayohifadhi
- Ushirikishwaji wa jamii katika kupanga matumizi ya fedha zitokanazo na misitu wanayohifadhi.
- Kiwango cha usawa katika kugawana faida zitokanazo na usimamizi shirikishi wa misitu
- Utawala wa sheria
- Jinsi ngazi za wilaya zinavyounga mkono usimamizi shirikishi wa misitu.

Matokeo ya mfumo huu yatasaidia kulinganisha jamii moja na nyingine au wilaya moja hadi nyingine katika masuala ya utawala bora ndani ya mipango ya usimamizi wa misitu na kuzifanya jamii kutambua matatizo au mapungufu mbalimbali yaliyopo na kutafuta mbinu za kuboresha hali hiyo.

Nani anafanya tathmini hii?

Tathmini hii inafanywa na WANAMJUMITA toka kwenye vijiji husika ambao si wajumbe wa serikali ya kijiji au wajumbe wa kamati ya maliasili/msitu ya kijiji. Watathmini hao wanachaguliwa kwenye mikutano mkuu ya mitandao chini ya uangalizi wa mratibu wa kanda au msaidizi wake. Watu wawili watachaguliwa kutoka kila kijiji kilichoteuliwa ndani ya mkutano mkuu wa mtandao, na kisha watathmini hao watapatiwa mafunzo na mratibu wa kanda husika ya jinsi ya kufanya mijadala hiyo na kukusanya takwimu. Baada ya kupata mafunzo na kufanyiwa majaribio, watathmini watakuwa tayari kwa kukusanya takwimu.

Utambulisho kwa uongozi wa kijiji

Baada ya kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kufanya mjadala na kukusanya takwimu, mtathmini atatakiwa kuchukua barua ya utambulisho toka kwa mratibu wa kanda inayoelezea lengo la zoezi zima pamoja na kumtambulisha yeye kwa uongozi wa serikali ya kijiji. Baada ya kupewa ruhusa na uongozi wa serikali ya kijiji ya kuendelea, mthathmini ataomba kufanya majadiliano na uongozi wa serikali ya kijiji (Mwenyekiti na Mtendaji) na viongozi wa kamati ya maliasili (Mwenyekiti na Katibu). Vile vile mtathmini ataomba apatiwe nyaraka mbalimbali zenye taarifa za misitu kama mpango wa usimamizi wa msitu, sheria ndogo za msitu, daftari la doria, daftari la faini, takwimu za mapato na matumizi, muhtasari wa vikao n.k. Na mwisho atafanya majadiliano na kikundi cha watu wasiozidi kumi kama taratibu za kuwachagua zilivyoainishwa hapo chini.

Jinsi ya kuchagua washiriki wa mjadala

- Tafadhli unaombwa kuchagua watu kumi (10) kijijini watakaoshiriki mjadala huu.
- Hakikisha kwamba, washiriki wa mjadala huu si wajumbe katika Kamati ya Maliasili/Msitu ya Kijiji au Serikali ya Kijiji.
- Hakikisha kwamba kila kitongoji kinatoa wawakilishi wake watakaohudhuria mjadala huu.
- Wajumbe watakaochaguliwa lazima wawe na uelewa kuhusu masuala ya uhifadhi wa misitu/maliasili kijijini (kwa mfano; wafunga nyuki, wanaohifadhi misitu yao binafsi, na wengineo)
- Wajumbe watakaochaguliwa lazima watoke katika nyumba (familia) tofauti, yaani nyumba moja itoe mtu mmoja tu.
- Uchaguzi wa wajumbe lazima uzingatie jinsia zote yaani kuwe na wanawake 5 na wanaume 5
- Andaa sehemu kwa ajili ya kufanyia mkutano huo
- Viongozi wa vijiji kama mwenyekiti wa kijiji na mtendaji hawataruhusiwa kuhudhuria mjadala huu bali watafanya mahojiano na mthathmini kwenye ofisi ya serikali ya kijiji.

Kanuni za uendeshaji mjadala au mambo ya kuzingatia wakati unapoendesha mjadala

1. Elezea na fafania lengo la mjadala huo kwa ufasaha zaidi na hakikisha wajumbe wanakuelewa vizuri kabla haujaendelea
2. Tumia lugha inayoeleweka kwa kila mjumbe, kama wajumbe wengi hawaelewi Kiswahili basi fafania swali kwa kutumia lugha ya asili iliyozeleka.

3. Epuka kutumia lugha za kitaalamu pale inapowezekana, endapo kuna umuhimu wa kutumia neno hilo basi hakikisha unalitolea ufafanuzi zaidi na wajumbe wanalielewa vizuri
4. Elezea kila swali kwa ufasaha na litolee ufafanuzi
5. Tengeneza mazingira ya kiurafiki zaidi kati yako na wahojiwa ili kupata majibu yenye ukweli.
6. Anza mjadala kwa maongezi ya kawaida kwa mfano; ulizia hali ya hewa ikoje, mavuno ya mazao mwaka huu yakoje n.k.
7. Kuwa makini sana na maswali yanayogusa hisia za wajumbe moja kwa moja, kama kuna swali la aina hiyo jaribu kuliuliza kwa njia nzuri na ya kirafiki zaidi.
8. Epuka kutumia maneno makali na ya kiubaguzi
9. Endapo mjumbe anaonekana kutoka nje ya mada inayozungumziwa, tafuta kauli nzuri itakayomrudisha kwenye mada bila kumfanya ajisikie vibaya
10. Epuka kuandika jibu la mtu mmoja, majibu yote yanayotolewa ni lazima yakubaliwe na washiriki wote kabla ya kuandikwa kwenye dodoso.
11. Hakikisha kila mshiriki anatoa mawazo yake na epuka mtu mmoja kutawala mjadala wote.

Jinsi ya kuwasilisha taarifa zilizokusanywa

Baada ya kukusanya taarifa hizi, tafadhali jaza majibu ya dodoso hilo kwenye nakala zingine tatu ili upate jumla ya nakala nne. Weka nakala moja iliyojazwa kikamilifu kwenye bahasha kubwa iliyoandaliwa na kuwekwa anuani ya posta na Mratibu wa kanda. Wasiliana na Mratibu wa kanda na umtumie nakala hiyo kwa njia ya posta. Nenda kwenye ofisi ya posta iliyo karibu na eneo unaloishi na utume nakala hiyo. Nakala ya pili ikabidhiwe kwenye uongozi wa serikali ya kijiji kwa ajili ya kumbukumbu za ofisi na nakala ya tatu ikabidhiwe kwenye uongozi wa Mtandao husika na nakala ya nne unatakiwa kubaki nayo ili itakapotokea kwamba taarifa uliyotuma haikufika basi nakala iliyobaki itumike.

Malipo kwa ajili ya chakula kwa washiriki

Kutakuwa na malipo kwa ajili ya chakula kwa watu wote watakaoshiriki zoezi hili, washiriki hao ni watu kumi (10) watakaoshiriki kwenye mjadala wa kikundi, viongozi toka serikali ya kijiji na Kamati ya maliasili 4 (Mwenyekiti wa kijiji, Mtendaji, Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya maliasili) na watathmini 2. Kila mtu atalipwa gharama ya shilingi 3,000/= za kitanzania kama gharama za chakula, maji na soda. Pesa hiyo atapewa mtathmini siku atakapokabidhiwa dodoso.

Kila Mtathmini atalipwa shilingi elfu kumi (10,000/=) kama malipo ya kufanya zoezi la kukusanya takwimu hizo. Zoezi hili linategemewa kufanyika kwa muda wa siku moja. Malipo kwa mtathmini

yatalipwa pale atakapokabidhiwa dodoso. Ni wajibu wa kila mtathmini kuhakikisha kwamba dodoso lililojazwa linamfikia Mratibu wa kanda kwa muda unaotakiwa.

Urudishwaji wa matokeo ya taarifa zilizokusanywa kwa wananchi

Taarifa toka kwenye dodoso lililojazwa zitafikishwa makao makuu ya ofisi ya MJUMITA na mratibu wa kanda kwa njia ya kuziingiza kwenye “database” iliyoandaliwa na Afisa teknolojia wa mradi. Takwimu hizo zitatolewa kwenye “database” na kufanyiwa uchambuzi na mwisho taarifa kamili itaandaliwa ikionyesha matokeo ya utawala bora kwa katika kila kijiji. Matokeo ya kila kijiji yatawasilishwa kwenye vijiji husika kwenye mikutano mikuu ya kijiji na jamii itapata fursa ya kujadili hali hiyo katika mkutano huo. Endapo jamii itaonyesha nia ya kufanya mabadiliko kwenye baadhi ya mambo basi utaratibu utapangwa wa jinsi ya kusaidia kutatua tatizo au mapungufu hayo.

Maelekezo kwa kila kipengele kilichopo kwenye dodoso

(Tafadhali tumia dodoso lililoambatanishwa kwenye mwongozo huu, hakikisha unajaza nakala tatu (3) za dodoso; Ofisi ya kanda nakala 1; Ofisi ya serikali ya kijiji nakala 1; Mtathmini nakala 1)

Tafadhali unaombwa kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye sanduku la maelekezo kwa kila kipengele au maelekezo yaliyopo kwenye swali yenye mwandiko wa mlalo na pia ufuate kama maelekezo hayo yatakavyokuagiza. Maelekezo hayo ni kwa ajili ya kumpa mtathmini maelezo ya ziada na hayatakiwi kusomwa kwa wajumbe wa mjadala

Sehemu ya kwanza

Sehemu ya kwanza kwenye dodoso ina lengo la kumtambulisha mtathmini, kufahamu idadi ya watu waliopo kijijini, kufahamu ukubwa wa eneo la msitu wa hifadhi ya kijiji na eneo la msitu lililo nje ya msitu wa kijiji. Pamoja na kufahamu muda unaotumika tangu mpango wa usimamizi wa msitu na sheria ndogo za msitu zinapofikishwa wilayani mpaka kupitishwa. Kipengele hiki kitajazwa kwa msaada wa viongozi wa serikali ya kijiji. Upatikanaji wa nyaraka za mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na sheria ndogo za msitu za kijiji zitakusaidia kujaza kipengele hicho. Utatakiwa kujaza kipengele A au B kutegemeana na aina ya usimamizi shirikishi wa msitu unaofanywa na kijiji husika. Kipengele A kitajazwa tu endapo kijiji husika kinatekeleza mpango wa uhifadhi shirikishi msitu wa hifadhi wa kijiji; kipengele B kitajazwa endapo kijiji kinatekeleza mpango wa uhifadhi shirikishi wa pamoja yani kati serikali/makampuni binafsi na jamii; na endapo kijiji kinatekeleza mipango yote miwili yaani mpango shirikishi msitu wa hifadhi wa kijiji na ule wa pamoja kati ya serikali/makampuni binafsi basi vipengele vyote viwili yaani A na B lazima vijazwe.

Sehemu ya pili

Sehemu hii ina lengo la kufahamu juhudi mbalimbali zinazofanywa na ngazi ya msitu wilaya na vyombo vya usalama kama polisi katika kuunga mkono juhudi za kijiji katika harakati za kutekeleza mipango ya uhifadhi shirikishi wa jamii. Maswali mbalimbali yanayopima utendaji kazi wa mamlaka

hizo mbili yameandaliwa ili yaulizwe kwa Mwenyekiti na mtendaji wa kijiji pamoja na katibu na mwenyekiti wa kamati ya maliasili ya kijiji. Tafadhali tembelea ofisi ya serikali ya kijiji ili uonane na viongozi hao na kufanya mahojiano nao kwa kufuata muongozo wa maswali ya kipengele cha pili.

Sehemu ya tatu

Kipengele hiki kina lengo la kutaka kufahamu kama kijiji kina utaratibu wa kutunza takwimu mbalimbali za shughuli zinazofanyika kijiji na hasa zinazohusu mipango ya uhifadhi wa misitu kijijini. Vile vile kufahamu mipango mbalimbali iliyopo kijiji inayohusu usimamizi wa misitu na jinsi inavyotekelezwa kwa kuzingatia utekelezaji wa sheria zilizowekwa katika kusimamia misitu hiyo. Tafadhali omba nyaraka mbalimbali toka kwenye serikali ya kijiji na katibu wa kamati ya maliasili kwa ajili ya kupata uhakika wa majibu ya taarifa ya maswali yaliyoandaliwa katika kipengele hicho.

Omba nyaraka ya **sheria ndogo za misitu, mpango wa usimamizi wa misitu kijijini, takwimu za doria, mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali za misitu na mihutasari ya vikao toka kamati ya maliasili na serikali ya kijiji**. Hakikisha kwamba kipengele hiki kinajazwa kwa umakini kwa kuangalia majibu ya maswali ya kila kipengele toka kwenye nyaraka husika na wala siyo kuuliza maswali kwa wahusika. Kama nyaraka hizo hazikupatikana, utatakiwa kujibu swali la kwanza katika kipengele hicho na utoe sababu za kukosekana kwa nyaraka hizo na uende kwenye kipengele kinachofuata.

Sehemu ya nne

Maswali ya kipengele hiki yameandaliwa kwa ajili ya kupata taarifa kutoka kwenye kikundi cha wanajamii hapa kijiji kwa njia ya mjadala. Majibu toka kwenye maswali hayo yatawezesha kufahamu jinsi jamii husika inavyoshirikishwa katika shughuli za usimamizi wa misitu kijijini; wananchi wanavyoshiriki kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu rasilimali za misitu, mawasiliano kati yao na uongozi wa kijiji pamoja na kuelewa kama kuna uwazi katika mipango ya pesa na kwenye nyaraka mbalimbali kijijini.

Tafadhali elezea kwa ufasaha lengo la zoezi hili kama lilivyoelezewa kwenye sehemu ya utangulizi. Waeleze kwamba ni ruksa kuuliza au kutaka maelezo ya ziada kama kuna swali halijaeleweka vizuri; majibu yote yatapewa uzito sawa; hakuna malipo au fidia itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayeshiriki katika mjadala huu bali ni kazi ya kujitolea; majina ya walioshiriki yatachukuliwa kama kumbukumbu ya ofisi ya MJUMITA na wala hayatatolewa kwa mtu mwingine yeyote na mwisho zoezi hili halina lengo la kunyoosheana vidole kwamba nani amesema nini nani ametenda nini bali kutafuta njia ya kuboresha kiwango cha utawala bora katika kijiji chenu.

DODOSO

Na: _____

SEHEMU YA KWANZA

TAARIFA ZA UTANGULIZI

Jina la Mtathmini: _____

Namba ya simu ya mtathmini: _____

Jina la Kijiji: _____

Idadi ya watu kijijini _____

Kata: _____

Wilaya: _____

Mkoa: _____

Ni aina gani ya usimamizi shirikishi wa misitu unaofanywa katika kijiji chenu?

- a. Usimamizi wa misitu wa hifadhi wa kijiji
- b. Usimamizi wa pamoja wa misitu kati ya serikali/makampuni binafsi na jamii

Jaza kipengele A kama kijiji chenu kina msitu wa hifadhi wa kijiji

A: USIMAMIZI WA MISITU WA HIFADHI WA KIJJI

No.	Jina la msitu	Ulianzishwa mwaka gani	Ukubwa wa msitu ndani ya kijiji chako (Ekari)	Mpango wa usimamizi wa msitu ulipelekwa wilayani lini?	Mpango wa msitu ulipitishwa wilayani mwaka gani	Sheria ndogo za maliasili zilipelekwa wilayani mwaka gani	Sheria ndogo za maliasili zilipitishwa mwaka gani
1.							
2.							
3.							
4.							

Jaza kipengele B kama kijiji chenu kinafanya usimamizi wa pamoja kati ya jamii na serikali kuu

B: USIMAMIZI WA PAMOJA WA MISITU KATI YA SERIKALI/MAKAMPUNI BINAFSI NA JAMII

No.	Jina la msitu	Mipango ya kushiriki kusimamia msitu wa pamoja ilianza mwaka gani	Sheria ndogo za kusimamia msitu wa pamoja zilipelekwa wilayani mwaka gani	Sheria ndogo za kusimamia msitu wa pamoja zilipitishwa na wilaya mwaka gani	Mkataba wa makubaliano kati ya kijiji na serikali kuu ulisainiwa lini?
1.					
2.					
3.					
4.					

C1. Ukubwa wa eneo la msitu ambalo halijahifadhiwa ndani ya kijiji

chako (Ekari)_____

C2. Je kijiji chako kina mpango uliokwishapitishwa wa matumizi bora

ya ardhi?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

SEHEMU YA PILI

MASWALI KWA VIONGOZI WA SERIKALI YA KIJJI NA KAMATI YA MSITU YA KIJJI

1. Je uvunaji wa rasilimali za misitu unaruhusiwa kufanyika kwenye msitu wowote kijiji kwa kibali
 - a) Ndiyo
 - b) Hapana (Kama hapana toa sababu_____)

Ruka swali namba 2 kama jibu la swali namba 1 hapo juu ni hapana

2. Kama jibu ni ndiyo, je ni sababu zipi hupelekea utolewaji wa vibali hivyo?
 - a) Vibali hutolewa kwa kila mtu na kwa sababu yeyote
 - b) Vibali hutolewa kutegemeana na mahitaji ya rasilimali za misitu waliyonayo watu
 - c) Idadi maalumu ya vibali hutolewa kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali kwa miaka ijayo.
 - d) Vibali hutolewa kama Serikali ya kijiji inahitaji mbao au miti kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kijiji kama vile shule, zahanati n.k.
 - e) Mengineyo_____
3. Ni mamlaka gani hupokea pesa zinazokusanywa toka kwenye ada au faini za misitu kwa sasa?
 - a) Kamati ya maliasili
 - b) Serikali ya kijiji
 - c) Halmashauri ya wilaya
 - d) Wanadoria wanaolipwa na kijiji
 - e) Wengineo_____
4. Mgawanyo wa mapato yatokanayo na ada au faini za msitu ukoje?
 - a) Asilimia 100 ya mapato huenda kwenye Kamati za maliasili
 - b) Asilimia 100 ya mapato huenda kwenye serikali ya kijiji
 - c) Asilimia fulani huenda kwenye kamati ya maliasili na nyingine serikali ya kijiji
 - d) Asilimia fulani hupelekwa wilayani, nyingine kwenye kamati ya maliasili na nyingine kwenye serikali ya kijiji
 - e) Asilimia fulani hupelekwa wilayani na nyingine kwenye serikali ya kijiji
 - f) Haifahamiki vizuri
 - g) Mengineyo_____
5. Je kijiji au wananchi wameshawahi kupeleka kesi inayohusu uharibifu wa misitu katika **ofisi ya misitu wilaya** ndani ya miezi 12 iliyopita? (*Zungushia majibu yaliyo sahihi*)

- a) Hapana, kwa sababu hawawezi au hawapendi kutoa msaada
- b) Hapana , kwa sababu hakuna shida
- c) Ndiyo

Kama jibu la swali namba 5 ni hapana basi ruka maswali namba 6,7, 8 na 9.

6. Ni matukio mangapi ya uhalifu wa misitu kijijini yalishawahi kupelekwa katika **ofisi ya misitu wilaya** na wananchi au uongozi wa kijiji ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita_____
7. Kati ya matukio yaliyotolewa taarifa katika **ofisi ya misitu wilaya**,je ni matukio mangapi yamefuatiliwa?_____
8. Kati ya matukio yaliyotolewa taarifa, je ni mara ngapi **ofisi ya misitu wilaya** imetoa adhabu kwa watu walioshiriki kwenye uhalifu_____
9. Kati ya matukio yaliyotolewa taarifa, je ni mara ngapi **ofisi ya misitu wilaya** imetoa adhabu kwa kufuata sheria?_____
10. Je kijiji au wananchi wameshawahi kupeleka kesi inayohusu uharibifu wa misitu **polisi** ndani ya miezi 12 iliyopita? (*Zungushia majibu yaliyo sahihi*)
- a) Hapana, kwa sababu hawawezi au hawapendi kutoa msaada
 - b) Hapana , kwa sababu hakuna shida
 - c) Ndiyo

Kama jibu La swali namba 10 ni hapana basi ruka swali namba 11, 12,13 na 14

11. Ni matukio mangapi ya uhalifu wa misitu kijijini yalishawahi kupelekwa **polisi** na wananchi au uongozi wa kijiji ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita_____
12. Kati ya matukio yaliyotolewa taarifa **polisi**,je ni matukio mangapi yamefuatiliwa na polisi?_____
13. Kati ya matukio yaliyotolewa taarifa **polisi**, je ni matukio mangapi yamefikishwa **mahakamani**?_____
14. Kati ya matukio yaliyotolewa taarifa **mahakani**, je ni matukio mangapi yametolewa hukumu _____
15. Je **ofisi ya msitu wilaya** ilitoa kibali cha uvunaji katika msitu wa kijiji chenu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?
- a) Ndiyo
 - b) Hapana

Kama jibu la swali namba 15 ni hapana ruka swali namba 16, 17, 18, 19, 20 na 21.

16. Je ofisi ya msitu wilaya imetoa vibali vingapi katika msitu wa kijiji chenu ndani ya miezi 12 iliyopita? _____
17. Je uongozi wa kijiji ulishiriki katika baraza la uvunaji la wilaya ili kufanya maamuzi ya kutoa vibali?
- Ndiyo, walishiriki kutoa kila kibali (idadi ___)
 - Ndiyo, walishiriki kutoa zaidi ya nusu ya vibali (idadi _____)
 - Ndiyo, wameshiriki kutoa chini ya nusu ya vibali (idadi _____)
 - Hapana, hawajashiriki katika kutoa kibali cha aina yeyote

Kama jibu la swali namba 17 ni hapana basi ruka swali namba 18

18. Kama jibu ni ndiyo, ni aina gani ya uongozi katika kijijini chenu ulioshiriki kwenye mkutano wa kamati ya uvunaji ya wilaya? (*Zungushia majibu sahihi*)
- Wajumbe wa serikali ya kijiji walishiriki
 - Wajumbe wa kamati ya maliasili kijijini walishiriki
 - Mtendaji na mwenyekiti wa Kijiji
 - Wengineo _____
19. Je vibali vilivyotolewa vimezingatia mpango wa usimamizi wa misitu kijijini?
- Ndiyo, vibali vyote vimezingatia mpango wa usimamizi misitu kijijini
 - Hapana, vibali vilivyotolewa vinakiuka mpango wa usimamizi misitu kijijini

Kama jibu la swali namba 19 ni hapana basi ruka swali namba 20

20. Je ni nini kilisababisha vibali vilivyotolewa kukiuka mpango wa usimamizi misitu kijijini?
- Uongozi wa kijiji haukushirikishwa
 - Mpango wa usimamizi wa misitu kijijini haukupitishwa na halmashauri ya wilaya
 - Uongozi wa kijiji ulishirikishwa lakini haukutoa taarifa wilayani kwamba kibali kinakiuka mpango wa usimamizi wa misitu.
 - Uongozi wa kijiji ulitoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa mpango wa usimamizi wa misitu ila taarifa hizo hazikushughulikiwa.
 - Mengineyo _____
21. Je ni faida gani jamii inapata kutokana na kutolewa kwa vibali kwenye msitu au ardhi ya kijiji chao?
- Kiasi cha pesa za ada ya uvunaji hubakishwa kwenye kijiji na zingine hupelekwa wilayani
 - Kiasi cha pesa hutolewa kama posho kwa wajumbe wanaoshiriki kupitisha kibali hicho
 - Hakuna pesa ya aina yeyote inayobaki kwa wananchi kutokana na vibali vinavyotolewa kijiji

d) Mengineyo_____

22. Ni taarifa zipi za rasilimali za misitu zinatolewa na ofisi ya misitu wilaya kwenye Serikali ya kijiji?

(Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)

a) Mipango ya uvunaji ya wilaya

b) Kiwango cha mapato kilichokusanywa na wilaya kutokana na ada au faini kwenye msitu wa kijiji au vijiji jirani.

c) Hakuna taarifa yoyote inayotolewa kwenye uongozi wa kijiji

d) Mengineyo_____

23. Je serikali ya kijiji ina akaunti ya benki?

a) Ndiyo

b) Hapana

24. Kama ndiyo, je pesa zipatikanazo toka kwenye rasilimali za misitu huwekwa kwenye akaunti hiyo?

a) Ndiyo

b) Hapana (Toa sababu_____)

25. Je kamati ya maliasili ya kijiji ina akaunti ya benki

a) Ndiyo

b) Hapana

26. Kama ndiyo, je pesa zipatikanazo toka kwenye rasilimali za misitu huwekwa kwenye akaunti hiyo?

a) Ndiyo

b) Hapana (Toa sababu_____)

SEHEMU YA TATU

KUHAKIKI TAARIFA TOKA KWENYE NYARAKA

Hakikisha unapata nyaraka husika ndipo ujaze sehemu hii, endapo nyaraka hizo hazikupatikana basi jaza swali la kwanza katika kipengele husika na ruka sehemu hii na uende inayofuata

MPANGO WA USIMAMZI WA MSITU WA KIJJI

Jaza kipengele hiki endapo tu umefanikiwa kupata mpango wa usimamizi wa msitu wa kijiji, kama hapana jaza swali namba 27 tu na uende kwenye kipengele kinachofuata (Zungushia jibu sahihi)

27. Je umefanikiwa kupata nakala ya mpango wa usimamizi wa misitu wa Kijiji?

- a) Ndiyo
- b) Hapana (Toa sababu _____)

28. Katika mpango wa usimamizi wa msitu kijijini, je kuna eneo lililotengwa kwa ajili ya uvunaji wa miti ya kwa ajili ya matumizi mbalimbali (kama mbao, miti ya kujengea, mkaa n.k)?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

29. Katika mpango wa usimamizi wa msitu kijijini, je kuna kiwango maalumu cha mazao ya misitu kinachoruhusiwa kuvunwa kwa mwaka?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

30. Katika mpango wa usimamizi wa msitu kijijini, je taratibu za uchaguzi wa Kamati ya maliasili zimeainishwa?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

31. Je, mpango wa usimamizi wa msitu unasemaje kuhusu taratibu za uchaguzi wa kuziba nafasi za wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji?

- a) Wanakamati kupendekeza au kuchagua wanakamati wapya ili kuziba nafasi hizo
- b) Tunasubiri mpaka uchaguzi ujao ndipo tuchague mtu mwingine
- c) Kupiga kura maalum katika mkutano mkuu ujao ili kuchagua wajumbe wa kujaza nafasi hizo
- d) Serikali ya kijiji kupendekeza wajumbe wapya wa kuziba nafasi hizo
- e) Hakuna kipengele kinachoelezea taratibu za uchaguzi wa kuziba nafasi za wajumbe wa kamati
- f) Mengineyo_____

32. Je kuna kipengele ndani ya mpango wa usimamizi wa msitu kinachoelezea majukumu ya kamati ya maliasili?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

SHERIA NDOGO ZA MISITU ZA KIJJI

Jaza nafasi hii tu kama umefanikiwa kupata nakala ya sheria ndogo za msitu, kama hakuna jaza swali namba 33 tu na uende kinachofuata. (Zungushia majibu sahihi)

33. Je umepata sheria ndogo za maliasili?

- a) Ndiyo
- b) Hapana(Toa sababu_____)

34. Kama ni ndiyo je, kuna kipengele ndani ya sheria ndogo ya msitu kinachoelezea, kama mtu akikamatwa mara nyingi akifanya uhalifu msituni faini yake huongezeka kutokana na idadi ya makosa aliyofanya?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

35. Je, kuna kipengele ndani ya sheria ndogo ya msitu kinachoelezea kwamba, faini ya mtu atakayekamatwa amekata miti 10 ni zaidi ya yule atakayekamatwa akikata mti mmoja?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

36. Ni sababu zipi zilizowekwa kisheria za kumuondoa mjumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji (Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)?

- a) Mjumbe wa kamati ya maliasili anaweza kuondolewa kwa sababu yeyote
- b) Wajumbe wa kamati ya maliasili wanaweza kuvuliwa nafasi zao endapo watahindwa kutekeleza majukumu yao
- c) Wajumbe wa kamati ya maliasili wanaweza kuondolewa endapo watapatikana na kosa la kupokea au kutoa rushwa.
- d) Hakuna sababu zilizoainishwa kisheria
- e) Mengineyo_____

TAARIFA /MIHTASARI YA VIKAO

Jaza sehemu hii tu kama umefanikiwa kupata nakala ya mihutasari ya vikao vya kamati ya maliasili na serikali ya kijiji, kama hakuna jibu swali namba 37 tu na uende kwenye kipengele kingine

37. Je umepata mihutasari ya vikao

- a) Ndiyo
- b) Hapana(Toa sababu_____)

38. Je kamati ya maliasili imekutana mara ngapi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? _____

39. Je kamati ya maliasili imefanya doria kwenye msitu mara ngapi ndani ya miezi 12 iliyopita? _____

40. Je serikali ya kijiji imefanya mikutano mikuu mara ngapi ndani ya miezi 12 iliyopita_____

TAKWIMU ZA DORIA, MAPATO NA MATUMIZI YA RASILIMALI ZA MISITU

Jaza kipengele hiki tu kama umefanikiwa kupata takwimu za doria, faini na ada, mapato na matumizi. Kama hukuna jaza swali namba 41 tu na uende kipengele kinachofuata (Zungushia jibu sahihi)

41. Je umepata nakala zinazoonyesha takwimu mbalimbali za kamati ya maliasili kama doria, faini, mapato na matumizi

- a) Ndiyo (Zitaje_____)
- b) Hapana (Toa sababu_____)

42. Je, Kamati ya misitu inatunza takwimu?

- a) Ndiyo
- b) Hapana (Toa sababu_____)

43. Kama jibu ni ndiyo, ni kwa jinsi gani takwimu za kamati ya maliasili zina uhalisia?

- a) Shughuli zote zinazofanywa na kamati zinawekwa kimaandishi
- b) Baadhi ya shughuli za kamati huwekwa kimaandishi
- c) Kamati haiweki kumbukumbu zozote
- d) Mengineyo_____

44. Ni aina gani ya takwimu zinazohifadhiwa na kamati ya misitu ya kijiji? (Zungushia majibu yaliyo sahihi)

- a) Mihutasari ya vikao vya kamati
- b) Tarehe ya kufanya doria
- c) Jina la kikundi kilichofanya doria

- d) Maelezo ya shughuli haramu zinazofanyika msituni na kuonekana
- e) Idadi ya watu waliokamatwa wakifanya uhalifu msituni
- f) Majina ya watu waliokamatwa wakifanya uhalifu msituni
- g) Kiwango cha mazao ya misitu kilichotaifishwa kutoka kwa wahalifu
- h) Faini iliyolipwa na watu waliokamatwa wakifanya uhalifu msituni
- i) Kiwango cha ada iliyolipwa kutokana na vibali vya uvunaji vilivyotolewa
- j) Mapato kwa ajili ya matumizi ya kamati ya maliasili
- k) Maelezo ya kina ya jinsi pesa zilivyotumika
- l) Stakabadhi za jinsi pesa zilivyotumika
- m) Mengineyo_____

45. Serikali ya kijiji inatunza takwimu gani zinazotokana na mapato toka kwenye misitu kama ada na faini? (*Zungushia majibu yaliyo sahihi*)

- a) Kiwango cha mapato
- b) Chanzo cha mapato
- c) Takwimu zinazohusu mapato na matumizi
- d) Mengineyo_____

SEHEMU YA NNE

MASWALI YA KUONGOZA MJADALA NA WANAKIKUNDI

**Tafadhali zungushia majibu yaliyo sahihi baada ya kupata jibu lililokubaliwa na washiriki wote waliohudhuria
mjadala**

46. Ni aina gani ya uhifadhi shirikishi uliopo kijijini kwenu? (Zungushia jibu sahihi)

- a) Usimamizi shirikishi msitu wa jamii
- b) Usimamizi shirikishi msitu wa pamoja
- c) Usimamizi shirikishi wa jamii na wa pamoja
- d) Mengineyo_____

**Uliza swali namba 47 kama kijiji kinatekeleza usimamizi shirikishi wa pamoja kati ya jamii na
serikali/makampuni binafsi**

47. Ni faida gani wananchi wanapata kutokana na usimamizi wa pamoja wa misitu kati ya serikali/makampuni binafsi na jamii "JFM" (Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)?

- a) Kugawana mazao ya misitu yaliyokamatwa au mapato yaliyotokana na mauzo ya mazao hayo
- b) Kugawana mapato yatokana na ada na faini za mazao ya msitu
- c) Ruhusa ya kuchota maji, kuokota kuni, kufuga nyuki, kuchuma dawa za miti shamba, kuchuma uyoga na matunda
- d) Kuvuna miti ya mbao kwa kiwango kilichopangwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kijiji kama vile shule, zahanati n.k
- e) Hakuna faida yeyote ipatikanayo kwa kuwepo kwa usimamizi wa pamoja wa msitu
- f) Mengineyo_____

Uliza swali namba 48 kama kijiji kinatekeleza usimamizi msitu wa hifadhi wa kijiji na jamii

48. Ni faida gani wananchi wanapata kutokana na kuwepo usimamizi msitu wa hifadhi wa kijiji (Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)?

- a) Kugawana mazao ya misitu yaliyokamatwa au mapato yaliyotokana na mauzo ya mazao hayo
- b) Kugawana mapato yatokanayo na faini zilizotozwa
- c) Ruhusa kupata matumizi ya kawaida ya msitu. Kama vile kuchotamaji, kuokota kuni, kufuga nyuki, kuchuma dawa za miti shamba, kuchuma uyoga na matunda pamoja na kulisha mifugo

d) Kuvuna miti ya mbao kwa kiwango kilichopangwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kijiji kama vile shule, zahanati n.k

e) Hakuna faida yoyote ipatikanayo kwa kuwepo kwa usimamizi wa pamoja wa msitu

f) Mengineyo _____

49. Je, ni nani wameshiriki katika kutoa mawazo/mchango wakati wa kutengeneza mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu kijijini (*Siyo kuupitisha tu*) Zungushia majibu yote yaliyo sahihi?

a) Serikali ya Kijiji

b) Kamati ya maliasili ya kijiji

c) Wananchi kwenye mkutano mkuu wa kijiji

d) Wananchi kwenye mikutano mkuu ya vitongoji

e) Wanamtandao wa MJUMITA

f) Watalaamu mbalimbali

g) Wengineo _____

50. Je kuna utaratibu wa kupitia na kuufanyia marekebisho mpango wa usimamizi wa msitu wa kijiji?

a) Ndiyo, mara _____ kwa mwaka

b) Hapana

c) Haifahamiki

51. Je msitu wa kijiji una mipaka?

a) Ndiyo

b) Hapana

52. Ni vitu gani mlivyotumia kuonyesha mipaka yenu msituni?(*Zungushia majibu sahihi*)

a) Vizuizi vya moto

b) Miti ya kupandwa

c) Kuchora alama

d) Mabango

e) Mawe ya mpaka(bikoni)

f) Mengineyo _____

Uliza swali namba 53 tu endapo kijiji kina sheria ndogo za usimamizi wa msitu wa kijiji

53. Nani alishirikishwa kutoa mawazo/mchango wakati wa kutengeneza sheria hizo (*siyo kuzipitisha tu*) Zungushia majibu yote yaliyo sahih?

- a) Serikali ya kijiji
- b) Kamati ya maliasili ya Kijiji
- c) Wananchi kwenye mkutano mkuu wa kijiji
- d) Wananchi kwenye mikutano mikuu ya vitongoji
- e) Wengineo _____

54. Je, mkutano mkuu umeitishwa mara ngapi ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita? _____

55. Kwa makadirio, ni watu wangapi walihudhuria mkutano mkuu wa kijiji kwa mara ya mwisho?

56. Je, mara nyingi mkutano mkuu wa kijiji huitishwa muda gani? _____

57. Je, asilimia ngapi ya watu waliohudhuria mkutano mkuu uliopita walikuwa ni wanawake?

- a) Ni zaidi ya asilimia 50 (Zaidi ya nusu ya watu waliohudhuria)
- b) Kama asilimia 50 (Nusu ya watu ya watu waliohudhuria)
- c) Zaidi ya asilimia 25 lakini ni chini ya asilimia 50 (Chini ya nusu ya watu waliohudhuria)
- d) Chini ya asilimia 25 (robo ya watu waliohudhuria)

58. Je sheria ndogo za misitu zimeshawahi kusomwa kwenye mkutano mkuu ndani ya miezi 12 iliyopita?

- a) Ndiyo
- b) Hapana (Toa sababu _____)

59. Je ni watu wangapi wanazifahamu sheria za misitu kijijini?

- a) Kila mtu
- b) Zaidi ya nusu ya watu
- c) Chini ya nusu ya watu
- d) Chini ya watu 45

60. Je ni taratibu gani zilitumika katika kuwachagua wajumbe wa kamati ya maliasili kijijini (*Zungushia majibu yote yaliyo sahihi*)?

- a) Kila kitongoji kilichagua wawakilishi wao kwenye mikutano mikuu ya vitongoji.
- b) Kila kitongoji kilichagua wagombea ambao walipitishwa na mkutano mkuu wa kijiji
- c) Serikali ya kijiji ilichagua wajumbe kutoka kila kitongoji na kupitishwa na wananchi katika mkutano mkuu wa kijiji.
- d) Serikali ya Kijiji iliwachagua wajumbe wa kamati ya maliasili.
- e) Hakuna kamati ya maliasili kijijini.
- f) Mengineyo _____
- g) Hatujui

61. Ni utaratibu gani wa upigaji kura hutumika katika kuchagua wajumbe wa kamati ya maliasili?

- a) Kunyoosha vidole
- b) Kura za siri
- c) Hatujui
- d) Mengineyo _____

62. Kamati ya maliasili hukaa madarakani muda gani kabla ya uchaguzi mwingine? _____

63. Je ni nani wanashiriki katika kufanya doria(*Zungushia majibu yote yaliyo sahihi*)?

- a) Kamati ya maliasili ya kijiji
- b) Kikundi cha wanadoria wanaolipwa(*Tofauti na wanakamati*)
- c) Wananchi wanaojitolea
- d) Wajumbe wa serikali ya kijiji
- e) Wengineo _____

64. Je, kuna uvunaji uhalifu wowote uliofanyika katika Msitu wa kijiji au kwenye msitu wa pamoja ndani ya miezi 12 iliyopita?

- a) Ndiyo (Idadi _____)
- b) Hapana

Kama jibu la swali namba 64 ni hapana ruka swali namba 65 na 66

65. Kama ni ndiyo, ni matukio mangapi ya uhalifu yalishughulikiwa ndani ya muda wa miezi 12 iliyopita na kupelekea mtu kuadhibiwa?(Mfano: kulipa faini au kufanya kazi za jamii)

- a) Asilimia 100 ya matukio ya uhalifu yalishughulikiwa na watu kupewa adhabu (Idadi ____)
- b) Zaidi ya nusu ya matukio yalishughulikiwa na watu kupewa adhabu (Idadi ____)
- c) Chini ya nusu ya matukio ya uhalifu ndiyo yalishughulikiwa na watu kuadhibiwa (Idadi ____)
- d) Hakuna adhabu iliyotolewa kutokana na uhalifu uliofanyika

66. Kama kuna adhabu iliyotolewa kwa kosa la uhalifu wa misitu ndani ya miezi 12 iliyopita, ni mara ngapi adhabu hizo zinafuata sheria ndogo za misitu?

- a) Asilimia 100 ya matukio ya uhalifu yameadhibiwa kwa kufuata sheria (Idadi ____)
- b) Zaidi ya nusu ya matukio ya uhalifu yameadhibiwa kwa kufuata sheria ndogo za misitu (Idadi ____)
- c) Chini ya nusu ya matukio ya uhalifu yameadhibiwa kwa kufuata sheria ndogo za misitu (Idadi ____)
- d) Hakuna adhabu iliyotolewa kwa kuzingatia sheria ndogo za misitu

67. Ukilinganisha na miaka ya nyuma na miezi 12 iliyopita, hali ya uvunaji haramu misitu ikoje?

- a) Iko vile vile

- b) Imeongezeka
- c) Imepungua

Uliza swali namba 68 endapo tu jibu la swali namba 67 ni c

68. Kama uvunaji haramu umepungua, je ni nini kimesababisha? *(Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)*
- a) Miti mizuri kwa ajili ya mbao na mkaa imebaki michache/imeisha
 - b) Kamati ya misitu imeongeza idadi ya doria/ inawajibika ipasavyo
 - c) Kushirikishwa kwa jamii katika kusimamia msitu
 - d) Serikali ya kijiji imeimarisha usimamizi wa sheria
 - e) Mamlaka ya wilaya imeimarisha usimamizi wa sheria
 - f) Mamlaka ya nchi yameimarisha usimamizi wa sheria
 - g) Mengineyo_____
69. Ni kwa jinsi gani wanajamii wanaweza kukosoa utendaji kazi wa wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji? *(Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)*
- a) Wananchi hawafahamu kama wana wajibu wa kukosoa utendaji kazi wa kamati ya maliasili ya kijiji
 - b) Kuhudhuria na kutoa mawazo kwenye vikao vya kamati ya maliasili
 - c) Kuhudhuria na kutoa mawazo kwenye mikutano mikuu ya kijiji
 - d) Kutoa mawazo na kuyapeleka kwenye sanduku la maoni la kijiji
 - e) Kutembelea ofisi ya serikali ya Kijiji
 - f) Mengineyo_____
70. Ni kwa jinsi gani takwimu za kamati ya maliasili zinafikishwa kwa wananchi? *(Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)*
- a) Hakuna takwimu zilizokwishawahi kutolewa kwa wananchi
 - b) Taarifa husomwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji
 - c) Taarifa hupelekwa kwenye halmashauri ya serikali ya kijiji
 - d) Taarifa hubandikwa kwenye mbao za matangazo za kijiji
 - e) Mengineyo_____
71. Ni aina gani ya taarifa za kamati ya maliasili zinatolewa kwa wananchi? *(Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)*
- a) Idadi ya doria zilizofanyika
 - b) Maelezo ya shughuli za uhalifu zinazofanyika msituni na zikaonekana
 - c) Idadi ya watu waliokamwa wakifanya uhalifu wa misitu
 - d) Majina ya watu waliokamatwa wakifanya uhalifu msituni

- e) Kiwango cha mazao ya misitu kilichotaifishwa kutoka kwa wahalifu
- f) Faini iliyolipwa na watu waliokamatwa wakifanya uhalifu wa msitu
- g) Kiwango cha ada iliyolipwa kutokana na vibali vya uvunaji
- h) Mapato na matumizi ya fedha itokanayo na rasilimali za misitu
- i) Maelezo ya kina ya jinsi pesa zilivyotumika
- j) Stakabadhi za jinsi pesa ilivyotumika
- k) Kiwango cha mapato
- l) Chanzo cha mapato
- m) Mengineyo_____

72. Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, je kamati ya maliasili imewasilisha mara ngapi takwimu/taarifa zake kwa wananchi?_____

73. Je serikali ya kijiji inawasilisha kwa wananchi taarifa za mapato inayopata kutokana na faini, ada au mauzo ya mazao ya misitu yaliyotaifishwa?

- a) Ndiyo
- b) Hapana(Toa sababu_____)

Kama jibu la swali namba 73 ni hapana, ruka swali namba 74 na 75

74. Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, je Serikali ya kijiji imewasilisha mara ngapi takwimu za mapato yatokanayo na misitu ?_____

75. Ni kwa jinsi gani Serikali ya kijiji huwasilisha taarifa zake zinazohusu mapato yatokanayo na mazao ya misitu?

- a) Taarifa husomwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji
- b) Taarifa hubandikwa kwenye mbao za matangazo za kijiji
- c) Mengineyo_____

76. Kwa sasa, nani hufanya maamuzi ya jinsi ya kutumia pesa zinazokusanywa toka kwenye ada au faini za misitu? (*Zungushia majibu yote yaliyo sahihi*)

- a) Kamati ya Msitu huamua jinsi ya kutumia asilimia yake
- b) Serikali ya kijiji huamua jinsi ya kutumia asilimia yake
- c) Mkutano mkuu wa kijiji hupitia na kuipitisha bajeti ya Serikali ya kijiji na kamati ya Msitu
- d) Mengineyo_____
- e) Haifahamiki vizuri

77. Je, wanajamii wana haki ya kugawana mapato yatokanayo na misitu kwa matumizi ya binafsi au familia?

- a) Ndiyo
- b) Hapana

78. Je mapato yatokanayo na rasilimali za misitu yametumikaje ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita?

(Zungushia majibu yote yaliyo sahihi)

- a) Malipo kwa ajili ya shughuli za uhifadhi
- b) Malipo kwa ajili ya matumizi ya serikali ya kijiji
- c) Malipo kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kijiji
- d) Malipo kwa watu au familia
- e) Mengineyo_____
- f) Haifahamiki

ORODHA YA WASHIRIKI WA MJADALA

Na.	Jina	Jinsia	Kitongoji	Anuani/Simu	Saini
1					
2					
3					
4					
5					
6					
7					
8					
9					
10					